

Mapokezi Ya Familia Ya Eil(Wanaojifunza Lugha Ya Kiingereza) / Itifaki Ya Usajili.

Usajili na mapokezi ya wanafunzi wageni katika wilaya ya shule ya katoliki ya Edmonton hufanyika katika One World...One Centre. Wanafunzi wote wageni, ambao lugha yao ya kwanza sio kiingereza watatathminiwa ili kudhibitisha ustadi wao katika lugha ya kiingereza na kiwango chao cha msaada kwa ajili ya programu ESL(Kiingereza kama lugha ya pili). Wafanyakazi wa Liaison watakusaidia wewe mwanafunzi kukamilisha nyaraka za usajilishaji kwa njia ipasavyo na pia kukupa maelezo maalum kuhusu aina za rasilimali na usaidizi ambayo shirika hili litatoa kwa minajili ya wanafunzi wageni na familia zao.

Fomu ambazo utapaswa kujaza ni kama;

- Fomu ya kusajili mwanafunzi
- Fomu ya ruhusa ya kutathmini ESL(kiingereza kama lugha ya pili)
- Fomu ya kusajili wanafunzi kwa kuzingatia taarifa za kimsingi kuhusu mtoto wako pamoja na masomo aliyoyapata hapo awali. Taarifa hii itamsaidia mwalimu kuweka mapango halisi katika mafunzo ya mtoto wako.
- Dodoso za kutathmini hitaji la familia. Hili litadhihirisha taarifa maalum kuhusu mipango ya jumua ambayo ni ya riba kwako. Ukosefu wa taarifa hii unaweza kukuzuia kutumia mipango hii ya jumua kwa namna ipasavyo.

Katika ukurasa wa 4 wa fomu ya usajili wa wanafunzi utahitajika kusoma na kutoa ridhaa na makubaliano yako panaposwa kwenye sehemu ifuatayo;

- **Makubaliano ya mwanafunzi kuwajibika katika matumizi ya rasilimali.**

Hati hii inaelezea majukumu anayo mtoto wako kuhusiana na utumizi wa rasilimali za kupasha habari zinazomilikiwa na shule ya katoliki ya Edmonton kama tarakilishi,intaneti na baruapepe.

- **Utumizi na ufichuaji wa habari za kibinafsi.**

Hati hii inaelezea jinsi ambavyo na wakati upi wafanyakazi wa shule wanaweza kusanya na kutumia habari za kibinafsi za mwana wako.

- **Miongozo ya utumizi wa tovuti ya wilaya.**

Hati hii inaeleza wakati upi na taarifa gani za kibinafsi zinazoweza chapishwa kwenye tovuti hii ya Wilaya.

- **Ridhaa ya kutumia na kushirikisha vyombo vya habari.**

Kabla ya wanafunzi kushiriki katika matukio yoyote ya shule, shule inapaswa kupata idhini kutoka kwa wazazi wao. Idhini inahitajika kwa sababu vitu vinavyochukuliwa kuwa vya kibinafsi na vya siri kama kazi ya wanafunzi na wanafunzi wenyewe binafsi wanaweza pigwa picha, wanaweza rekodiwa kwenye video na wazazi, wageni au watendakazi wa vyombo vya habari.Habari hizi hutumika kusheherekea mafanikio ya wanafunzi na pia kutoa maelezo kuhusu elimu katika shule za katoliki na kazi inayofanywa na bodi ya shule za katoliki.

Tafadhali tenga wakati wako kusoma sehemu zote kwa makini na kutia alama sehemu zote unazokubaliana nazo.Iwapo utabadilisha mawazo yako, una fursa ya kuiondoa ridhaa yako wakati wowote.

- **Idhini ya kuwasiliana kwa njia ya elektoniki.**

Katika ukurasa wa 4 upande wa chini inaeleza kuwa shule za katoliki za Edmonton zinahitaji idhini yako kutumia barua pepe kama njia ya kuwasilisha habari kuhusu shule au wilaya.



Baadhi ya mawasiliano haya ni kama habari kuhusu vitu vinavyopeanwa shuleni kwa nafuu, matangazo ya kukuza mipango na shughuli zinazoendelea shule kama; mpango wa chakula cha mchana, upigaji picha au matukio yoyote yanayofanyika shuleni. Hatutakuwa na uwezo wa kukupasha habari hizi kwa njia ya elektroniki bila idhini yako. Iwapo utaamua kutoidhinisha, utapokea ujumbe ya mahudhurio na za dharura tu.

Ili kusajilisha mtoto wako, unahitajika kutoa maelezo yafuatayo

1. Ushahidi wa hali ya uhamiaji wa mwanafunzi – aidha maoja ya;
 - Kadi ya makazi ya kudumu ya mwanafunzi na mmoja wa wazazi wake au uthibitisho wa kuwa mkaazi wa kudumu.
 - Kibali cha kufanya kazi au kusoma ya mzazi pamoja na kibali cha ugeni au kusoma cha mwanafunzi kama kinapatikana.
 - Hati ya kudai ulinzi wa mkimbizi au ilani ya uamuzi katika mkataba ya wakimbizi.
 - Kibali cha kusoma cha mwanafunzi (wanafunzi wanaosoma nchi nyingine pasi na yao).
2. Cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi.
3. Cheti cha ubatizo, iwapo mwanafunzi ni mkatoliki na pia kama cheti hiki kinapatikana.
4. Ushahidi wa ulezi wa mwanafunzi. Ushahidi huu unahitajika iwapo mwanafunzi hajahitimu miaka kumi na nane (18) na haishi na mzazi wake.
5. Hati ya kudhibitisha anwani ya nyumba anapoishi kama; leseni ya dereva, vyeti vya matumizi ya kilasiku, mkataba kwa ukodeshaji au hati yoyote ambayo lina jina na anwani lako.

Ili kutenga miadi au kupata maelezo zaidi kuhusu mchakato wa usajili na nyaraka zinazohitajika, tafadhali piga simu kwa (jina lako), Akol, Akol at One World...One Centre kwa 780-944-2001, ext. 5106.